MKUKUTA II

VIPAUMBELE

MDAHALO KUHUSU SERA ZA KITAIFA TAREHE 2-8 DECEMBER 2010,

BLUE PEARL UBUNGO PLAZA

YALIYOMO

- Utangulizi
- Mwelekeo
- Misingi ya Vipaumbele
- Vipaumbele

UTANGULIZI

UTANGULIZI

- MKUKUTA II: 2011 - 2015:
  - Uliandaliwa kwa kuzingatia matokeo ya tafiti mbalimbali, maoni ya wadau na makundi yote;
  - Unazingatia matokeo (outcome based), katika maeneo makuu matatu:
    - Ukuaji uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato,
    - Ubora wa maisha na ustawi wa jamii, na
    - Utawala Bora na Ustawi wa Jamii
  - Unasistiza mchango wa ukuaji uchumi na utawala bora na uwajibikaji katika kupunguza umaskini,
  - Kuendelea kuzingatia masuala mtambuka,
- Umezingatia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, na Malengo ya Maendeleo ya Milenia-2015

MWELEKEO

MWELEKEO

- Mambo mapya katika MKUKUTA II,
  - Msisitizo katika maeneo machache ya kipaumbele,
  - Misisitizo katika ukuaji wa sekta zenye tija na zinazoajiri watu wengi zaidi (Drivers of growth),
  - Uwekeza katika kuboresha kiwango cha ubora wa huduma za jamii (elimu, afya na maji),
  - Kukuza rasilimali watu ili kuchangia katika ukuaji uchumi na ushindani katika uchumi,
  - Msisitizo katika usimamizi wa uchumi na kujenga mazingira bora ya uwekezaji na biashara,
  - Ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi na huduma bora kwa jamii - dhana ya “Public Private P’ship –PPP”

MISINGI YA VIPAUMBELE

MISINGI YA VIPAUMBELE

- Vipaumbele vilivyoainishwa vimezingatia mambo yafuatayo:
  1. Kuendeleza njia kuu za uzalishaji (i.e, rasilimali watu, ardhi, mtaji, na technolojia),
  2. Kujenga na kuimarisha taasisi za kusimamia uchumi na ustawi wa jamii,
  3. Kujenga na kuimarisha miundo mbinu ya uchumi;-(i.e,umeme, reli, bandari, viwanja vya ndege, barabara za vijijini, na njia za mawasiliano), na
  4. Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Taifa

VIPAUMBELE

VIPAUMBELE

a) Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato:
   i. **Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi**: kuendeleza sekta ndogo ya mazao, mifugo na uvuvi kwa kuboresha mfumo mzima wa uzalishaji (usambazaji wa pembejeo, miundo mbinu ya umwagiliaji, maghala, wataalam, mikopo, matumizi bora ya ardhi, na masoko);
   ii. **Sekta ya Viwanda**: kuendeleza viwanda vitakavyotumia rasilimali za ndani, kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na kilimo, maliasili kama vile misitu, na madini, Viwanda vya pembejeo nk; kuendeleza viwanda mama; kuendeleza kanda maalumu za uzalishaji (Special Economic Zones & Export Processing Zones)

VIPAUMBELE.. INAEND..

(a) **Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini:**

iii. **Sekta ya Fedha:** kuimarisha huduma ya fedha ili kupanua upatikanaji wa mikopo nafuu ya kilimo, biashara na uwekezaji;

iv. **Sekta ya madini:** kujenga viwanda vya kuongeza thamani, upatikanaji wa vifaa kwa wachimbaji wadogo, upatikanaji teknolojia kwa wachimbaji wadogo, kuimarisha taasisi za utafiti na usimamizi wa madini - sheria mpya ya madini inakamilishwa,

v. **Sekta ya Utalii:** kuibua na kuendeleza vivutio vya utalii, kujenga uwezo wa kitaalamu, kujenga miundo mbinu, kuimarisha sheria na haki miliki nk,

VIPAUMBELE.. INAEND..

(a) Kukuza uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato:

vi **Miundombinu,** barabara za vijijini, reli, bandari, viwanja vya ndege, nishati ya umeme na miundombinu ya mawasiliano na habari, usafirishaji wa nishati ya mafuta na gesi n.k.

vii. **Dhana ya PPP:** Kupanua na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi kwa kupitia utaratibu wa “Public Private Partnership (PPP)” katika kujenga miundombinu kama vile, nishati mbadala, reli, viwanda, bandari, kupanua uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, utoaji wa huduma za jamii (afya, elimu na mafunzo) na huduma za kifedha.

viii. **Soko la Pamoja la Afrika Mashariki**: Kuimarisha uwezo wa kushiriki katika shirikisho la Afrika ya Mashariki na Kusini mwa Afrika. Hii ni pamoja na kukuza elimu na ujuzi kuhimili ushindani wa masoko.

VIPAUMBELE.. INAEND..

(a) Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato:

ix **Ardhi na Makazi:** kuimarisha na kupanua mfumo wa taarifa za ardhi; kuanzisha vituo vya kitaifa vitakavyosaidia upimaji wa ardhi na uchoraji ramani; kuboresha matumizi bora ya ardhi vijijini na mijini; na kuanzisha na kusimamia mikopo ya nyumba.

x. **Vitambulisho vya Kitaifa:** Kukamilisha na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa utambuzi na usajili wa raia (National Identification and Registration of Persons)

VIPAUMBELE..INAEND..

(b) Ubora wa Maisha na Ustawi wa jamii

i. **Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari:**
   - Kuinua kiwango cha ubora wa elimu,
   - Kuwekeza katika miundo mbinu ya kielimu, vifaa vya kusomea na kufundishia,

ii. **Elimu ya Ufundi na ya Juu:**
   - Kupanua vyuo vya ufundi,(VETA, Polytechnics),
   - Kuhuisha mtaala wa vyuo vya ufundi sambamba na mahitaji ya sekta ya uchumi na soko la kimataifa,
   - Kuboresha vyuo vikuu hasa vya sayansi,

VIPAUMBELE..INAENDELEA

(b) Ubora wa Maisha na Ustawi wa jamii:

iv. **Afya:**

- Kuimarisha mifumo ya utoaji huduma(health delivery system)
- Kufundisha na kuajiri wataalam wa afya hasa madaktari na wakunga,
- Kuimarisha vyuo vya tiba ya afya na elimu ya sayansi kuanzia ngazi ya chini,

v. **Maji safi na taka:**

- Kupanua na kujenga miundo mbinu ya uvunaji maji
- Kujenga miundo mbinu ya usambazaji maji,
- Kulinda na kutunza vyanzo vya maji,
- Kupanua miundo mbinu ya maji taka, na ukusanyaji taka

VIPAUMBELE ...INAENDELEA

(c) Utawala bora na uwajibikaji:

i. Kuimarisha utekelezaji wa maboresho katika sekta ya utumishi wa umma, sheria, Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa, na usimamizi wa fedha za umma;
ii. Kuboresha na kuhakikisha demokrasia, utawala bora, haki za binadamu na utawala wa sheria
iii. Kuendeleza amani, utulivu wa kisiasa, mshikamano na umoja wa kitaifa
iv. Kuhakikisha uwajibikaji na uongozi bora;
v. Kujenga moyo wa umoja, utaifa na upendo,
vi. Kuimarisha mifumo ya kupambana na rushwa.

Asanteni
Kwa Kunisikiliza